



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UCHUKUZI  
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHIN



## TAARIFA KWA UMMA

### MKURUGENZI MKUU LATRA ATOA POLE KWA MKUU WA MKOA LINDI

*Dar es Salaam, Tarehe 22 Aprili, 2024*

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), CPA Habibu Suluo, ametoa salamu za pole kwa Mhe. Zainab R. Telack, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, kufuatia vifo vya watu 11 na majeruhi 08 vilivyotokana na ajali iliyotokea leo Jumatatu, tarehe 22 Aprili, 2024, majira ya saa 07:30 mchana katika eneo la kijiji cha Somanga, kata ya Somanga, tarafa ya Mitinje, barabara kuu ya Lindi - Kibiti.

Ajali hiyo imehusisha gari la mizigo lenye namba za usajili T224 DZT, aina ya Howo yenye leseni ya LATRA namba C3A316637 iliyotolewa tarehe 15 Julai, 2023 na muda wake utamalizika tarehe 14 Julai, 2024 pamoja na tela lake lenye namba za usajili T920 CUK yenye leseni ya LATRA namba C8A308112 iliyotolewa tarehe 23 Juni, 2023 na muda wake utamalizika tarehe 22 Juni, 2024, mali ya Kampuni ya *Specialised Hauliers Ltd* iliyokuwa ikiendeshwa na Bw. Abdallah Hamis Dulazi (37), mkazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam.

Gari hilo lilikuwa likitokea mkoani Lindi kuelekea Dar es Salaam na liligongana na gari la abiria lenye namba za usajili T707 DSX aina ya Mazda lenye leseni ya usafirishaji ya LATRA namba A1A241394 iliyotolewa tarehe 27 Aprili, 2023 na muda wake utamalizika tarehe 26 Aprili, 2024 likitoa huduma ya usafiri njia ya Kilwa Kivinje - Somanga kupitia Nangurukuru. Gari hili, T707 DSX, lilikuwa likiendeshwa na Bw. Said Issa Mnokoto - mkazi wa Somanga na lilikuwa likitoka Somanga kuelekea Nangurukuru.

Chanzo cha ajali hiyo ni matumizi mabaya ya barabara yaliyosababishwa na dereva aliyekuwa anaendesha lori lenye namba namba za usajili T224 DZT Howo ambaye alihama ghafla kutoka upande wake wa kushoto na kwenda upande wa kulia na kugonga gari dogo la abiria na kusababisha ajali hiyo iliyosababisha vifo na majeruhi.

Katika salamu zake, CPA Suluo ametoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na wafiwa wote; vilevile amewapa pole majeruhi na kuwaomba uponaji wa haraka. LATRA inawataka madereva wote kufuata na kuzingatia Sheria na Taratibu za usalama barabarani ili kuepuka ajali zinazogharimu uhai na mali za Watanzania.

Salum Pazy  
Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano